Muhtasari wa Kituo cha Watoto wachanga cha Thames View

Kutoka kwa Wafanyikazi na Wasimamizi wote, karibu kwa shule yetu ya tamaduni anuwai.

Hapa kuna muhtasari wa maelezo muhimu na ya maana kwa ajili yako.

Tufahamishe ikiwa unahitaji msaada na utafsiri na tutakuelekeza kwa mtu ambaye anaweza kukalimani kwa ajili yako. Mara kwa mara wazazi wetu wanataka kuwasaidia wazazi wengine kwa njia hii.

Sifa Zetu



Katika Kituo cha Watoto Wachanga cha Thames View tunafanya kazi ili kuwapa shule ya jamii inayojali, inayofurahisha na inayosaidia ambapo kila mtoto na familia yake ni wa maana.

Tunatoa mazingira ya kusoma, ambapo kila mtu anafikia uwezo wake kamili, haijalishi mahali anapoanzia.

Tunawafunza watoto kuheshimu, kukubali na kuthamini wanafunzi wenzao na watu wazima katika jamii ya shule ya tamaduni anuwai na katika maisha yao nje ya shule kwa kuwa mifano.



Tunataka watoto wafurahiye muda wao shuleni na waunde mazingira salama na mema ambapo wanahisi wanashughulikiwa, na wanathaminiwa kwa kukuza kujitegemea, imani na uwezo wa watoto wa kufanya maamuzi kivyao.

Tunalenga kufanya jamii ya shule yetu inayokaribisha na ya kirafiki na tunahisi kwamba ni muhimu kwamba wazazi na waalimu wafanye kazi kwa pamoja ili kuwasaidia na kuwaunga mkono watoto.

Kwa kuwa tunataka kusaidia familia zetu kupata matokeo mema kwa muda wanao na sisi, tunaendesha pia huduma mbalimbali ambazo zinaongeza yale shule inaweza kutoa na siku ya shule.

Pia, tunafanya kazi kwa karibu na wataalamu wote muhimu tunaoshirikiana nao katika mtaa na tunajivunia viungo vyetu vyema. Hii inajumuisha Kituo cha Watoto cha Sue Bramley, Kituo cha Shule ya Watoto cha Sue Bramley, Kituo cha Matibabu cha Thames View, Shule ya Watoto ya Christchurch, Huduma za Jamii, Shule zilizo karibu na huduma za elimu na msaada katika utawala.

Kwa pamoja tunatoa mtandao mzuri wa msaada kwa familia na toleo kamili 'lililounganishwa.'

Masaa ya Shule

Shule ya watoto	**Miaka 3-4**	Saa tatu na dakika kumi hadi saa tano na dakika arobaini asubuhi na saa sita na dakika aroboaini na tano hadi saa tisa na robo mchana
Upokeaji	**Miaka 4-5**	Saa tatu na dakika kumi hadi saa tano na dakika arobaini na tano asubuhi na saa saba hadi saa tisa na robo mchana
Mwaka 1 na Miaka 2	**Miaka 5-6 Miaka 6-7**	Saa tatu na dakika kumi asubuhi hadi saa sita na robo mchana na saa saba na robo hadi saa tisa na robo mchana

Tafadhali jaribu kuhakikisha mtoto wako hajachelewa. Kila darasa huanza siku na shughuli za kusoma au kuhesabu na mtoto wako atakosa mafunzo muhimu akichelewa.

Lenga kuwasili dakika 5 kabla ya shule kuanza, kwa kuwa hautakuwa ukisubiri kwa muda mrefu, haswa siku zenye baridi.

Ukumbi umefunguliwa kila asubuhi kwa watoto ambao wanataka kuhudhuria Klabu ya Kiamsha kinywa ambayo inaanza kuanzia saa mbili na nusu asubuhi. Watoto wanaangaliwa na wafanyikazi wa shule. kuna ada ndogo.

Ukichelewa, tafadhali usimweke mtoto wako nyumbani siku hiyo – ni vyema kwetu mtoto kuchelewa badala ya kutokuja kabisa. Unapowasili shuleni utahitaji kuona mfanyikazi aliye ofisini, ili uhakikishe mahudhurio ya mtoto wako yameandikwa na chakula cha jioni kimeagizwa.

Uvumbuzi wa Shule

Kama 'shule iliyoongezwa', tunawapa watoto klabu ya shule ya kiamsha kinywa na vilabu mbalimbali vya shughuli za jioni, ambavyo watoto wanaweza kuhudhuria kwa ada ndogo. Hii inajumuisha mafunzo ya umahiri wa kadanda, densi na kompyuta.

Pia tuna mshauri wa msaada kwa wazazi, ambaye anaendesha vikundi vya aina yote vya wazazi, na anaweza kukupa msaada juu ya shida nyingi za kila siku ambazo familia zinakabaliana nazo. Njoo na ushiriki wasiwasi wowote unao kabla uwe mkubwa zaidi.

Tuna kompyuta/wavuti kwa Wazazi na Walezi mnamo Jumatatu asubuhi. Huendelea kuanzia saa tatu na nusu hadi saa nne na nusu asubuhi. Kompyuta za kupakatwa zilizo na uwezo wa wavuti hutolea na msaada unapatikana pia.

Meneja wetu wa Ufundi atajibu maswali yoyote yanayohusiana na kompyuta ambayo unayo na kompyuta yako ya nyumbani. Njoo na uzungumze na yeye na atafanya awezavyo ili kukusaidia na kukupa msaada wa busara.

Ili kukusaidia kukujilisha kuhusu kinachojiri shuleni na kutatua shida za barua za shule kupotea zikiwa njiani kuelekea nyumbani kutoka shuleni, tunapeana barua kwa huduma ya barua pepe. Ili kujiandikisha, wazazi wanapaswa kutuma barua pepe iliyo na jina la mtoto kwa:

Newsletter.TVI@bdcs.org.uk



Daima ni vyema kukutana 'uso-kwa-uso' na waalimu wetu, haswa wakati wa kuzungumzia kuhusu mafunzo. Walakini, tunafahamu kwamba maisha ya wazazi inawezakuwa na shughuli sana na wakati mwingine ni vigumu kupata muda wa kuongea. Ikiwa wewe, au mtoto wako mna swali kuhusu kazi ya nyumbani au unahitaji msaada juu ya kusoma nyumbani, unaweza kutuma barua pepe kwa:

HomeworkHelp.TVI@bdcs.org.uk

Waalimu wetu watajaribu kujibu swali lako, au kuweka miadi ili kukusaidia zaidi kwa wakati unaofaa.

Mahudhurio

Ni hitaji la kisheria kwamba watoto wahudhurie shule mara kwa mara, na kwamba wazazi wao au walezi wanastahili kuhakikisha hii inafanyika. Kutokuhudhuria kwa aina yoyote, isipokuwa wakati wa ugonjwa, hakuhimizwi.

Haupaswi kwenda likizo za familia wakati wa masaa ya shule.

Tarehe zetu zote za shule zinapatikana kwenye tovuti yetu:
http://www.thamesview-i.bardaglea.org.uk/diarydates.htm

Lakini, ikiwa unazingatia kumtoa mtoto wako shuleni kwa ajili ya likizo, lazima uchukue fomu na ujaze kutoka kwa ofisi ya shule. Likizo zinazochukua zaidi ya wiki mbili hurekodiwa kama kutokuwepo kusioruhusiwa.

Ikiwa mtoto wako hataki kwenda shuleni basi zungumza nasi. Kunawezakuwa na sababu na tutafanya kazi kwa pamoja ili kusaidia kutatua shida hiyo.

Mahudhurio ya mara kwa mara na kuzingatia masaa ni muhimu sana kwa watoto kufaulu shuleni.

Ninastahili kufanya nini ikiwa mtoto wangu ni mgonjwa?

Ikiwa mtoto wako kwa kweli ni mgonjwa sana anastahili kubaki nyumbani na kupata nafuu kitandani.

Ikiwa ni hivi, tunakuomba upige simu kwa (020 8270 4317) au tuma ujumbe wa maandishi kwa (07943 922 655) kwa ofisi yetu ya shule kabla ya saa nne asubuhi kila siku ambayo hayuko na utuambie jinsi anavyoendelea.

Tunatoa mazingira ya kujali na ya kusaidia sana, na yanaweza kumsaidia mtoto wako kurudi shule mapema kwa njia nyingi:

- Kutoa dawa zilizoagizwa kwa mtoto wako (ukikamilisha fomu maalum kutoka ofisini)

- Kumwangalia mtoto wako kwa 'makini' anapokuwa akipona na kukufahamisha 'jinsi anavyoendelea'.
- Kuongea na daktari katika Kituo kilicho karibu cha Matibabu cha Thames View



- Kumpa chaguo tofauti wakati wa vyakula vya mchana (kwa mpangilio maalum)
- Kufanya kazi na wewe na mtoto wako ikiwa haponi au ikiwa anashida ya kufika shuleni kila asubuhi
- Kumsaidia kufikia kazi ambazo amekosa.

"Mahudhurio mema" ni nini?

Kwa sababu inaweza kuharibu elimu ya mtoto akikosa kwenda shuleni mara kwa mara, Serikali imewekea shule zote Lengo la Kitaifa la Mahudhurio ambapo wanafunzi wanastahili kuhudhuria asilimia 95 ya vikao vyote.

Hii inamaanisha kwamba, kwa mwaka, watoto wanastahili kukosa *kwa wastani* <u>siku 1 ya shule kwa mwezi</u> (au siku nusu kwa wiki mbili).

Tayari katika Kituo cha Watoto wachanga cha Thames View watoto wengi uhudhuria shule kila siku na wana mahudhurio ya asilimia 100.

Kila muhula tunatuza familia zetu zote ambazo zinafikisha Mahudhurio ya asilimia 100 na "Mkusanyiko wa Maua" maalum na maarifu sana.

Kila muhula, tunatuza mtoto baisikeli ambaye ameonyesha maendeleo mema katika kuhudhuria kwake kwa mwaka mzima hadi sasa.



Nitajua aje mahudhurio ya mtoto wangu?

Tunafanya kazi kwa ushirikiano na familia zetu, na kama shule, tunaendelea kuangalia mahudhurio. Mara kwa mara utajua kama mahudhurio ya mtoto wako yameshuka kwa sababu kwa wakati fulani, tutakuwa tumezungumza pamoja.

Kwa utaratibu, kila wiki mbili, tunachunguza kirasmi mahudhurio ya watoto wetu wote. Kila muhula, tunamwandikia kila mzazi ikiwa mahudhurio ya mtoto wao yamepungua chini ya kiwango cha haja:

- ✖ Chini ya asilimia 95 (kutokuwepo kwa siku nusu kila wiki mbili)
- ✖ Chini ya asilimia 90 (siku nusu kwa wiki)
- ✖ Chini ya asilimia 85 (karibu siku moja kwa wiki)
- ✖ Chini ya asimilia 75 (karibu siku moja na nusu kwa wiki)

Ijapokuwa mahudhurio ya 'asilimia 90' kwa wakati inaonekana kuwa juu, kwa wakati wote wa elimu ya mtoto, asilimia 10 iliyokosekana ni sawa na kupoteza mwaka mzima wa shule. Kwa kukufahamisha kupitia kwa barua, tunaweza kufanya kazi kwa pamoja ili kusaidia kuboresha mahudhurio ya mtoto wako na ufanisi kama mwanafunzi.

Athari za mahudhurio ya chini ni nini?

Kutohudhuria shule mara kwa mara kunaweza haribu elimu ya mtoto wako. Kitwakimu, ni watoto waliyo na mahudhurio ya asilimia 90 ndiyo wanapata gredi nzuri za mitihani na wana uwezekano wa kupata kazi nzuri baadaye maishani.

Watoto waliyo na mahudhurio duni wana shida ya kuhisi wamejumuishwa katika maisha ya shule na wanakuwa na ugumu wa kupata marafiki.

Watoto huona ni vigumu zaidi 'kufikia' kazi ambazo wamekosa ikiwa hawako mara kwa mara

Mara kwa mara, ni watoto ambao hawahudhurii mara kwa mara ambao wa kama wanaoathirika sana.

Mamlaka ya Mtaa wa Barking na Dagenham ya Mji wa London itashtaki familia ambazo zinashindwa kuhakikisha kwamba watoto wanahudhuria shule mara kwa mara, kwa kuwa ni hatia. Wazazi/Walezi wanaweza kupigwa faini, au kupelekwa kortini, kuhudhuria madarasa ya uzazi au hata kufungwa kwa kesi ambazo ni mbaya.

Hatutaki hii ifanyike kwa familia yoyote ya wanafunzi wa Kituo cha Watoto cha Thames View.



Shule yetu ina mazingira ya kujali na ya furaya, na kwa kuwa ina orodh kubwa ya wanaosubiri, sio haki kwa familia hizo ambazo zinatak kuwatuma watoto kwa shule yetu, lakini hawawezi kwa sababu imejaa.

Mipangilio ya Kuchukuliwa

Tuna idadi iliyowekwa ya nafasi katika kila kikundi cha mwaka.

Ikiwa hakuna maombi zaidi kwa nafasi za shule inayozidisha idadi inayoweza kuchukuliwa, basi Utawala wa Mitaa inaweza kuwachukua watoto wote ambao wanahitaji nafasi. Wakati kuna maombi zaidi ya nafasi, basi Utawala wa Mitaa itahitaji kuwa na kigezo cha uchukuaji ili kuamua ni nani anatapa nafasi na nani hatapata. Kigezo cha uchukuaji ni kama ifuatavyo:

1. "Watoto waliyoshughulikiwa".
2. Watoto waliyo na ndugu au dada anayehudhuria shule au Shule ya Watoto ya Thames View.
3. Watoto wanaoishi katika eneo lililopewa kipaumbele cha uchukuaji. (Hili ni Eleo la Mtaa lililotengwa na Utawala wa Mitaa kama lililopewa kipaumbele cha uchukuaji kwa shule maalum.)
4. Watoto wanaoishi karibu na shule kulingana na kipimo cha njia ya kutembea iliyokaribu inayopatikana.

Watoto ambao hawatapewa nafasi majina yao yatawekwa kwenye orodha ya wanaosuburi nafasi.

Taratibu za Malalamiko

Mwalimu Mkuu au Wasimamizi wa Shule watashughulikia malalamiko yote kuhusu masuala ya shule.

Jinsi ya Kuendelea:



Hatua ya 1
Katika visa vingi, daima ni bora kuanzia na kuibua suala lolote au wasiwasi moja kwa moja na mwalimu wa darasa la mtoto wako. Kutoelewana kwingi huwa mara kwa mara sio kwa kutaka na waalimu wetu watakusikiliza na kufanya wawezavyo ili kutatua suala hilo.

Hatua ya 2
Ikiwa bado unataka, wasiliana na shule ili ujadili shida yako au malalamiko. Ofisi ya shule itaweza kukusaidia katika kufanya mipango ya kukutana na Mwalimu mkuu msaidizi au Mwalimu mkuu. Katika visa vingi malalamiko yako yatashughulikiwa hadi uridhike.

Hatua ya 3
Walakini, ikiwa utataka kepeleka malalamiko yako mbele zaidi, wasiliana na Mwenyekiti wa Chombo Kinachosimamia shule, kupitia Ofisi ya Shule.

Hatua ya 4
Ikiwa shida/malalamiko yako hayajatatuliwa tafadhali andika malalamiko yako kwa Mkurugenzi wa Huduma za Watoto, ukitoa maelezo ya hatua ambazo tayari umechukua. Ni kusudi la Mkurugenzi wa Huduma za Watoto kufanya kazi kwa karibu na wazazi, shule na Wasimamizi ili kujaribu kusaidia kupata suluhu la shida.

London Borough of Barking & Dagenham

Tunatumaini kwamba utapata maelezo haya kuwa ya maana. Walakini, inakueleza tu kuhusu baadhi ya mambo tunayofanya katika shule yetu - kwa hivyo tafadhali njoo na uulize katika Ofisi ya Shule kuhusu kitu chochote unachotaka kujua, kama vile sare na jinsi ya kupata vyakula vya bure.

Maelezo zaidi yanapatikana kwenye tovuti ya shule yetu:
http://www.thamesview-i.bardaglea.org.uk/